# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Tel: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


*Unapojibu tafadhali taja*:
Kumb Na: NBS/S.40/21/455

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe:15 Agosti, 2011

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI JULAI, 2011

### Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye namna ya ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kutengeneza Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index formula" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 13.0

### Jedwali 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa mwezi Julai 2011 (Septemba 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Julai-2010 | Juni-2011 | Julai -2011 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 99.91 | 113.83 | 115.75 | 1.7 | 15.9 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 99.54 | 103.93 | 104.48 | 0.5 | 5.0 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 97.83 | 106.09 | 106.98 | 0.8 | 9.4 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 97.50 | 114.29 | 118.29 | 3.5 | 21.3 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 98.41 | 112.09 | 112.68 | 0.5 | 14.5 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 100.25 | 101.72 | 101.83 | 0.1 | 1.6 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 100.24 | 108.87 | 110.18 | 1.2 | 9.9 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 99.52 | 97.44 | 98.15 | 0.7 | -1.4 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 97.56 | 100.35 | 100.62 | 0.3 | 3.1 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 101.48 | 105.79 | 105.79 | 0.0 | 4.2 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 101.83 | 107.69 | 108.76 | 1.0 | 6.8 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 99.81 | 101.42 | 103.26 | 1.8 | 3.5 |
| | **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | **100.0** | **99.56** | **110.79** | **112.51** | **1.5** | **13.0** |
| **Makundi mengine teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 100.12 | 113.16 | 114.98 | 1.6 | 14.8 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 95.77 | 121.16 | 128.50 | 6.1 | 34.2 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 98.88 | 107.98 | 109.57 | 1.5 | 10.8 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 99.35 | 106.00 | 106.73 | 0.7 | 7.4 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa wa mwaka unapima kiwango cha badiliko la bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwezi Julai 2011 umeongezeka hadi asilimia 13.0 ikilinganishwa na asilimia 10.9 kwa mwaka ulioishia mwezi Juni 2011. Kwa ujumla Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 112.51 mwezi Julai 2011 kutoka 99.56 mwezi Julai 2010. Vyakula na vinywaji baridi vimeongezeka hadi asilimia 15.9 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2011 kutoka asilimia 12.3 mwezi Juni 2011.

### Mfumuko wa bei kwa bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula

Badiliko la Fahirisi ya bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limeongezeka hadi asilimia 14.8 kwa mwaka ulioishia Julai 2011 ikilinganishwa na asilimia 11.7 kwa mwaka ulioishia Juni 2011. Badiliko la bidhaa zisizo za vyakula limeongezeka hadi asilimia 10.8 kwa mwaka ulioishia Julai 2011 kutoka asilimia 10.0 kwa mwaka ulioishia Juni 2011.


### Mfumuko wa bei wa bidhaa na huduma zote isipokuwa bidhaa za vyakula na nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya

kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa watunga sera.

Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwaka ulioishia Julai 2011 umeongezeka hadi asilimia 7.4 kutoka asilimia 7.2 kwa mwaka ulioishia Juni 2011. Mfumuko wa bei wa nishati umeongezeka hadi asilimia 34.2 kwa mwaka unaoishia Julai 2011 kutoka asilimia 29.0 mwezi Juni 2011.

**Kielelezo 1: MWELEKEO WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA NA MFUMUKO WA BEI KUTOKA JULAI, 2010 HADI JULAI, 2011. (SEPTEMBA 2010 = 100)**




Kielelezo 1 hapo juu kinaonesha kumekuwa na mwenendo imara wa fahirisi za bei za taifa kutoka mwezi Julai 2010 hadi Novemba 2010. Fahirisi zinaonesha kuongezeka sana kwenye miezi ya Desemba 2010 hadi Julai 2011. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei umekuwa ukipungua hadi asilimia 4.2 mwezi Oktoba 2010 na umeanza kuongezeka hadi kufikia asilimia 13.0 mwezi Julai 2011.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 1.5

Mfumuko wa bei wa mwezi Julai 2011 umeongezeka kwa asilimia 1.5, Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 112.51 mwezi Julai 2011 kutoka 110.79 mwezi Juni 2011. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na mchele kwa asilimia 2.3, Mahindi kwa asilimia 4.3, unga wa mahindi kwa asilimia 2.6, unga wa ngano kwa asilimia 3.2, nyama ng'ombe kwa asilimia 3.1, nyama ya nguruwe kwa asilimia 3.5, dagaa kwa asilimia 3.8, samaki wakavu kwa asilimia 5.8, matunda kwa asilimia 0.6 na sukari kwa asilimia 2.1.


Bidhaa zisizo za vyakula zilizoongezeka bei ni pamoja na vitambaa vya nguo kwa asilimia 1.4, mafuta ya taa kwa asilimia 14.2, mkaa kwa asilimia 0.4, vifaa vya malazi kwa asilimia 1.1, vifaa vya umeme kwa matumizi ya nyumbani kwa asilimia 2.3, dizeli kwa asilimia 1.0, petroli kwa asilimia 0.4, huduma za usafirishaji wa abiria kwa asilimia 1.7 na huduma za mtandao wa komputa kwa asilimia 17.9.

**Thamani ya Shilingi 100 mwezi Septemba 2010 ikilinganishwa na mwezi Julai 2011**

Thamani ya shilingi 100 imepungua kutoka mwezi Septemba 2010 hadi kufikia shilingi 85 na senti 22 mwezi Julai 2011.

## MIENENDO YA BEI

**Kielelezo 2: Mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za bei**




Kielelezo namba 2 hapo juu kinaonesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei; fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi cha miezi tisa iliyopita zikilinganisha na fahirisi zingine isipokuwa kwa mwezi Aprili mpaka Julai 2011, kwa upande mwingine kundi la nishati na mafuta limekuwa na fahirisi za juu kuliko makundi mengine katika kipindi hicho. Kwa kipindi cha miezi 12, kundi la nishati na mafuta limeonesha kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**